UQAB
Jarida la



*Toleo 31 - Dhul-Qa'ada 1440 H / Agosti 2019 Miladi*

**Siri ya Mapenzi, Utulivu na Heshima ndani ya Maisha ya Ndoa**

**Miezi Mitatu Mitukufu Inafuatana**

**Mama Mmoja na Watoto 6 Wachanga Wanafariki kila Saa 2 ndani ya Yemen!**

**Nidhamu ya Elimu ya Msingi**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi - Halaqa 23**

**SWALI/JAWABU: Uhasama Kati ya Marekani na Iran**



# Merekebisho Kwenye Kanuni za Kuzuia Ugaidi ni Hatua Nyengine ya Kuushambulia Uislamu

بسم الله الرحمن الرحيم

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 12/1440 H | Ijumapili, 11 Dhul-Qa'ada 1440 H | 14/07/2019 M

# Merekebisho Kwenye Kanuni za Kuzuia Ugaidi ni Hatua Nyengine ya Kuushambulia Uislamu

## Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Tarehe 5 Julai, 2019 Rais Uhuru Kenyatta alitia saini mswada wa kanuni ya Sheria zilizofanyiwa marekebisho jumla ya mwaka 2019 ikiwemo ile kanuni ya kuzuia ugaidi (The Statute Law (Miscellaneous Amendment) Act 2019 – No. 21 of 2019). Hatua hii inamaanisha kuanzia sasa Huduma ya Kitaifa ya Polisi, Wizara ya Masuala ya Kigeni, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma, Huduma ya Wanyama Pori, Huduma za Magereza na Mamlaka ya Usafiri wa Angani zimejumuishwa na kuwa wanachama wa Kituo cha Kupambana na Ugaidi. Hii ni sambamba na mswada wa marekebisho wa sharia ya kuzuia ugaidi (Prevention of Terrorism (Ammendment) Bill, 2018 unaopendekeza kuhakikisha kuwa bodi za shule na mashirika ya kibinafsi pamoja na ya kidini yanashirikiana pamoja na asasi za serikali katika kusimamia utekelezwaji wa mipango maalum ya kupambana na mafunzo ya itikadi kali. Lau ukipita mswada huu basi wasimamizi wa shule watahitajika kuweka na kusasisha (update) kumbukumbu za wanafunzi wote shuleni, kuhakikisha kuwa walimu wanahamasishwa kufuatilia na kutambua itikadi kali miongoni mwa wanafunzi. Fauka ya hayo, kuna mswada mwengine wa marekebisho ya kifungu nambari 30 cha sheria ya kuzuia ugaidi unaopendekeza vifungo vya vya kuanzia miaka ishirini na thelathini kwa watakao kuwa na hatia ya matendo ya ugaidi.

Kulingana na maelezo ya kanuni hizi tungependa kufafanua yafuatayo:

'Vita dhidi ya ugaidi' nchini vinachukua sura pana zaidi inayohatarisha usalama jumla wa raia hususan jamii ya Waislamu nchini Kenya ambayo ndio inayolengwa zaidi katika kampeni jumla dhidi ya 'ugaidi'. Licha ya kuwa polisi wa Kenya kuwa na rekodi mbaya za ukiukwaji wa haki msingi za raia, twaona kupitia kanuni hizi serikali imewaongeza nguvu zaidi ambazo twahisi kuwa polisi pamoja na asasi za kiusalama zilizojumuishwa zitakandamiza jamii ya Waislamu.

Kuhusishwa shule, mashirika ya kibinafsi na makundi ya kidini kwenye mchakato wa vita dhidi ya 'ugaidi' na kile kiitwacho itikadi kali ni kuibua wasiwasi na hofu baina ya Waislamu ili waweze kufanyiana ujasusi wao kwao jambo ambalo Uislamu umelikataza. Na twatahadharisha wazazi na walimu Waislamu na washika wadau wa mashirika mbalimbali ya kidini wasije wakaingia katika kazi inayofanywa na maadui wa Uislamu kote ulimwenguni ya kuupiga vita Uislamu kwani kufanya hivyo kutawapelekea kupata idhlali hapa duniani na kesho akhera kukabiliwa na adhabu kali. Tunakumbusha kila Muislamu kwenye taasisi yoyote ile sawa ya serikali au ya kibinafsi kuwa anawajibika kuwa balozi wa ulinganizi safi wa Uislamu usiotumia njia za uhuni, fujo na mabavu kama njia ya kuleta mabadiliko. Waislamu mahala popote pale wanawajibika kuhami na kulinda utambulisho wa Uislamu.

Tafsir ya matamshi ya itikadi kali na misimamo mikali zapaswa kutiliwa shaka na kupigwa darubini kwani twaona kwamba matamshi hutumika mara nyingi katika kubana ufahamu wa Uislamu kuwa ni dini ya kiroho tu wala sio kimfumo. Isitoshe twahisi misamiati hii itazuia Waislamu kutoshikamana na mafunzo yao ya Kidini bali kuhofia pia kuzungumza na kuzilingania rai za Uislamu kuhusu jamii, uchumi na siasa. Na haya yote itakuwa pia ni kukiuka hata zile ziitwazo haki msingi za kibinadamu za uhuru wa itikadi na uhuru wa maoni kama zinavyoelezwa kwenye katiba ya nchi. Tunafahamu kuwa licha ya Kenya kusheheheni wanasiasa waovu wanaochochea raia kuleta vurugu kwa maslahi yao ya kisiasa, twaona wanasiasa hao kattu hawashtakiwi kwa kuwa na misimamo mikali au itikadi kali!

Kama tunavyoendelea kukariri kuwa sheria hizi za kupambana na ugaidi zinalenga si mwengine isipokuwa jamii ya Waislamu. Hakika sheria hizi ni sehemu ya kampeni ya kiulimwengu inayoongozwa na Marekani ya kushambulia fikra za Kiislamu. Fauka ya hayo zinapitishwa ili kuweza kutia hofu katika mioyo ya Waislamu ili wawache Uislamu na kuwatia mihemko ili kubeba fikra ovu za kisekula ambazo zinakwenda kinyume na Dini yao, Kampeni hii inalenga kuweka kizuizi kwa Uislamu usiweze kuongoza dunia katika ulingo wa kisiasa, kiuchumi, kijamii na kielimu kupitia hivi karibuni kusimama kwa Khilafah kwa njia ya Mtume (saw) ambayo wakati wake unakaribia kwa kasi mno. In Shaa Allah.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi Kwa Vyombo Vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

# Siri ya Mapenzi, Utulivu na Heshima ndani ya Maisha ya Ndoa

Moja kati ya mahusiano adhimu ambayo Mwenyezi Mungu (swt) amewawekea wanadamu ni mahusiano kati ya mwanamume na mwanamke. Mahusiano haya ndio asili ya mahusiano yote yanayounda familia. Hivyo basi ni muhimu yaweko katika hali nzuri yenye kupelekea kufaulu. Mwenyezi Mungu (stw) asema:

هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَجَعَلَ مِنْهَا زَوْجَهَا لِيَسْكُنَ إِلَيْهَا

"Yeye ndiye aliye kuumbeni katika nafsi moja; katika hiyo hiyo akamfanya mwenzi wake, ili akae naye kwa utulivu." [7:189]

Mwenyezi Mungu (swt) ameweka muongozo kwa mambo yote ya wanadamu, ili watu waweze kuondokana na dhiki na kupata njia iliyo nyooka. Wataweza kufaulu au kufeli katika dunia na watazawadiwa au kuadhibiwa huko akhera kwa mujibu wa kujifunga kwao na muongozo huo. Moja ya sababu ya kwa nini familia ya Kiislamu inafaulu ni kwa kuweko na muundo makini ambapo kila mwanachama wa familia anajua dori yake. Jambo zuri zaidi kuhusiana na mahusiano ya kijamii katika Uislamu ni kwamba mtu anatenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (swt), ima ni mahusiano baina ya mume na mke, wazazi na watoto au mahusiano ya kifamilia. Kuyatekeleza kwa mujibu wa Maamrisho ya Mwenyezi Mungu (swt) ni jukumu muhimu la Kiislamu na ambalo litazalisha mapenzi, utulivu na heshima ndani ya ndoa na muundo wa familia.

Mtume (saw) alikuwa na mahusiano ya karibu mno na wake zake na familia yake. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِمَنْ كَانَ يَرْجُو اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا

"Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana." [33:21]

Ibn Maja amesimulia kwamba Mtume (saw) alisema: خَيْرُكُمْ خَيْرُكُمْ لأَهْلِهِ وَأَنَا خَيْرُكُمْ لأَهْلِي "Walio bora miongoni mwenu ni wale walio bora kwa wake zao, na Mimi ni mbora kwenu kwa wake zangu."

Katika ndoa za Mtume (saw) kulikuweko na mapenzi, utulivu na heshima. Mtume (saw) alikuwa mwema kwa wake zake na sio dikteta, kwani uadilifu ni jukumu muhimu la mwanamume kwa mkewe. Alikuwa na mahusiano mema nao, alicheza nao, aliwafanyia dhihaka, aliwasaidia katika kazi zao za nyumbani alipokuwa na nafasi na kuwafunza masomo. Imesimuliwa na al Bukhari "Kila mara alijiunga nao katika kazi za nyumbani na wakati mwingine akishona nguo zake, viatu vyake na kufagia sakafu. Alikuwa akikama, akiwafunga na kuwalisha wanyama wake na kufanya kazi za nyumbani." Mtume (saw) alikuwa ngao na mlinzi wa wake zake, kama alivyosema Mwenyezi Mungu (swt):ِءاَسّنلا ىَلَع َنوُماّوَق ُلاَجّرلا

"Wanaume ni ngao na walinzi wa wanawake." [4:34]

Fauka ya hayo, Mtume (saw) alisisitiza usimamizi mwema na uliojaa makini kwa watoto na wazee. Yeye (saw) alisema: «لَيْسَ مِنَّا مَنْ لَمْ يَرْحَمْ صَغِيرَنَا وَيَعْرِفْ شَرَفَ كَبِيرِنَا»"Yeyote asiyewahurumia watoto wala kuwaheshimu wazee, sio katika sisi." (Abu Dawood, Al-Tirmidhi) Na asema Mwenyezi Mungu (swt):

وَقَضَى رَبُّكَ أَلاَّ تَعْبُدُواْ إِلاَّ إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا إِمَّا يَبْلُغَنَّ عِندَكَ الْكِبَرَ أَحَدُهُمَا أَوْ كِلاَهُمَا فَلاَ تَقُل لَّهُمَآ أُفٍّ وَلاَ تَنْهَرْهُمَا وَقُل لَّهُمَا قَوْلاً كَرِيمًا * وَاخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ الذُّلِّ مِنَ الرَّحْمَةِ وَقُل رَّبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيَانِي صَغِيرًا

"Na wazazi wawili muwatendee wema. Mmoja wao akifikia uzee, naye yuko kwako, au wote wawili, basi usimwambie hata: Ah! Wala usiwakemee. Na sema nao kwa msemo wa hishima. Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa kuwaonea huruma. Na useme: Mola wangu Mlezi! Warehemu kama walivyo nilea utotoni." [17:23-24]

Sifa kuu ya mwanamke ambaye mwanamume atapata furaha na amani ni Imani yake. Mtume (saw) alisema:«تُنْكَحُ الْمَرْأَةُ لأَرْبَعٍ لِمَالِهَا وَلِحَسَبِهَا وَلِجَمَالِهَا وَلِدِينِهَا فَاظْفَرْ بِذَاتِ الدِّينِ تَرِبَتْ يَدَاكَ»"Mwanamke anaolewa kwa moja ya sababu nne: utajiri wake, cheo chake, uzuri wake na kujifunga kwake na dini. Basi oa mwanamke mwenye dini, au kinyume chake utafeli." (Saheeh Al-Bukhari)

Mwanamke mchamungu anaona moja ya majukumu yake makuu ndani ya ndoa ni kumtwii na kumfurahisha mumewe kwa kuwa ni jukumu aliloamrishwa na Mwenyezi Mungu (swt). Haimaanishi kattu kwamba mwanamke asiwe na maoni yake na asijadiliane na mumewe au kutoa ushauri juu ya masuala. Bali inamaanisha kuwa lazima amkubali mumewe kama mtoa maamuzi wa nyumba na kujitahidi kuweza kufaulisha hilo. Jukumu hilo halimdunishi mwanamke mbele ya mwanamume, lakini ni jukumu ambalo ndani yake anapata malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu kama anavyopata malipo mwanamume anapokuwa mwema na kumtendea wema mkewe na kumpa malezi bora kwa kadri ya uwezo wake. Mtume (saw) alisema: إذا باتت المرأة هاجرة فراش زوجها لعنتها الملائكة حتى تصبح "Lau mwanamke atakuwa kando na kitanda cha mumewe usiku mzima basi Malaika walamlaani mpaka atakaporudi." Na yeye (saw) alimuuliza mwanamke:«أَذَاتُ بَعْلٍ أَنْتِ؟» قُلْتُ: نَعَمْ، قَالَ: «...فَإِنَّهُ جَنَّتُكِ وَنَارُكِ» "Una mume?" Akajibu: 'Naam.' Akasema: "….Basi yeye ni Pepo (Jannah) yako na Moto (Nar) wako."

Ni ushahidi kutoka kwa mwenendo wa Mtume kwamba kuchunga haki na majukumu baina ya wanandoa hupelekea kufaulu kwa ndoa na natija yake ni amani katika maisha ya familia pamoja na ulezi wa watoto na uwiano wa mahusiano ya kifamilia. Hivyo basi, Mtume (saw) ndio kiigizo chema kwa Waislamu katika masuala yote maishani. Kwa sababu Mtume (saw) anaonyesha kwamba Taqwa na ikhlass ni katika kutekeleza sheria za Mwenyezi Mungu katika njia iliyo bora. Yeye (saw) anatuonyesha namna ya kuweza kujitoa mhanga na namna ya kutokuwa mtumwa wa matamanio na kiburi. Kwa hiyo, ikiwa Muislamu mwanamume au mwanamke atatekeleza majukumu yake katika ndoa na kumpa mwandani wake haki zake kiukamilifu, basi Mwenyezi Mungu atatia mapenzi, utulivu na heshima pande zote mbili katika ndoa yao.

لَيْسَ الْبِرَّ أَنْ تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ وَآتَى الْمَالَ عَلَىٰ حُبِّهِ ذَوِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسَاكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَالسَّائِلِينَ وَفِي الرِّقَابِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَآتَى الزَّكَاةَ وَالْمُوفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَاهَدُوا وَالصَّابِرِينَ فِي الْبَأْسَاءِ وَالضَّرَّاءِ وَحِينَ الْبَأْسِ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ صَدَقُوا وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ

"Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika ukombozi wa watumwa na akawa anashika Sala, na akatoa Zaka, na wanao timiza ahadi yao wanapo ahidi, na wanao vumilia katika shida na dhara na wakati wa vita; hao ndio walio sadikisha, na hao ndio wajilindao." [2: 177]

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Amanah Abed**

# Miezi Mitatu Mitukufu Inafuatana: Tujipindeni Kufanya Kheri ikiwemo Kheri Kubwa ya Kufanya Kazi ya Kuleta Mageuzi Msingi

Mwenyezi Mungu (swt) amesema:

**(إِنَّ عِدَّةَ ٱلشُّهُورِ عِندَ ٱللَّهِ ٱثۡنَا عَشَرَ شَهۡرًا فِى كِتَـٰبِ ٱللَّهِ يَوۡمَ خَلَقَ ٱلسَّمَـٰوَٲتِ وَٱلۡأَرۡضَ مِنۡهَآ أَرۡبَعَةٌ حُرُمٌۚ ذَٲلِكَ ٱلدِّينُ ٱلۡقَيِّمُۚ فَلَا تَظۡلِمُواْ فِيهِنَّ أَنفُسَكُمۡ)**
“Hakika idadi ya miezi kwa Mwenyezi Mungu ni miezi kumi na mbili katika hukumu ya Mwenyezi Mungu tangu alipoumba mbingu na ardhi. Katika hiyo iko mitukufu. Hiyo ndiyo Dini iliyo sawa. Basi msidhulumu nafsi zenu.” [At-Taubah: 36]

Imepokewa kutoka kwa Abu Bakr (ra) kwamba Mtume (saw) alisema:

“Mgawanyiko wa wakati umerudi katika asili yake kama ilivyo sasa namna Mwenyezi Mungu alivyoziumba mbingu na ardhi. Mwaka una miezi kumi na mbili kati ya hiyo minne ni mitukufu. Mitatu inafuatana Dhul-Qa’da, Dhul-Hijja na Muharram, na wa nne ni Rajab (wa kabila) la Mudar unaokuja baina ya Jumada II na Shaaban.”
[Sahih Bukhari]

Imepokewa kutoka kwa Abu Sa’eed (ra) kwamba Mtume (saw) alisema:

“Leo sio siku tukufu katika siku zenu tukufu, mwezi huu sio mtukufu katika miezi yenu mitukufu, ardhi hii sio tukufu katika ardhi zenu tukufu? Damu zenu na mali zenu ni tukufu kama ilivyo siku yenu hii ya leo ndani ya mwezi huu wenu. Je nimefikisha (ujumbe)?’ Wakajibu: “Ndio.” Akasema: “Ewe Mwenyezi Mungu, shuhudia.”
[Ibn Majah]

Tukijaaliwa kufika Ijumaa ijayo tutakuwa tumo ndani ya mwezi mtukufu wa Dhul-Qa’da ambao ukimalizika unakuja Dhul-Hijja mwezi wa mwisho katika kalenda yetu tukufu ya Kiislamu nao pia ni mtukufu. Na baada yake utafuata mwezi wa kwanza wa Muharram nao pia ni mtukufu. Hakika itakuwa ni fursa ya kipekee kuweza kuishuhudia miezi hiyo ambayo ndani yake kila jema unalolifanya linakuwa na ubora mara dufu mbele ya Mwenyezi Mungu (swt). Na miongoni mwa mema ya kupatiliza ni kuiendea mbio kadhia nyeti ya kurudisha tena maisha ya Kiislamu kwa kufanya kazi ya kusimamisha serikali ya Kiislamu ya Khilafah kwa njia ya Utume ndani ya moja ya nchi za Waislamu katika ulimwengu wa Waislamu. Mbio hizi ni pamoja na kuusoma Uislamu kwa sura ya kimfumo, kuufahamu, kuutekeleza na kuulingania ili uweze kuchukua nafasi ya mfumo batili wa kisekula wa kirasilimali unao tawala dunia leo na ambao unaendeleza ukandamizaji, umwagaji damu na uporaji wa rasilimali za Waislamu na wasiokuwa Waislamu katika kila pembe ya dunia.

Ni katika miezi hii mitukufu sisi Waislamu ndipo tunapotakiwa kuzidisha juhudi zetu za ulinganizi wa kusimamisha Khilafah kwa kuwa ni ahadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt) na bishara kutoka kwa Mtume (saw). Kinyume chake ni hasara kubwa kwa kila ambaye yuko mbioni kuweka vikwazo kwa da’wah hii ikiwemo kushirikiana na watawala vibaraka ndani ya ulimwengu wa Waislamu na usiokuwa wa Waislamu ili kuwapotosha watu ili wabakie katika kiza cha ukafiri na kutawaliwa kwa mujibu wa sera na sheria zilizochorwa kwa mikono ya wakoloni Wamagharibi na kupitishwa na mabunge au mabaraza ya vibaraka wao duniani kote kwa sura ya kupambana na Ugaidi au Magaidi, Uislamu/Waislamu wenye Siasa Kali au au Uislamu/Waislamu wenye Misimamo Mikali. Ni hasara iliyoje kutangaza vita na Mwenyezi Mungu (swt) ndani ya miezi yake mitukufu kwa kwenda kinyume na ahadi yake na bishara ya mtume wake!

Hakika ni kupitia kusimama kwa Khilafah ndipo Waislamu na wasiokuwa Waislamu ulimwenguni watakapohisi kwa mara ya kwanza utulivu, maendeleo na ufanisi wa kweli baada ya takribani miaka 98H sawa na 95M tangu kuvunjwa kwa dola ya Kiislamu ya Khilafah mnamo 28 Rajab 1342H sawa na 3 Machi 1924M kwa mikono ya vibaraka wa Wamagharibi hususan kina Sharif Hussein na Mustafa Kamal, aliyekuwa myahudi kafiri.

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

**Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنكُمْ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِى ٱلْأَرْضِ كَمَا ٱسْتَخْلَفَ
ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ ٱلَّذِى ٱرْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ
يَعْبُدُونَنِى لَا يُشْرِكُونَ بِى شَيْـًٔا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْفَٰسِقُونَ﴾

حزب التحرير

HIZB UT TAHRIR

KUMB: 35/1440 Jumanne, 14 Shawwal 1440 H 18/06/2019 M

# Mama Mmoja na Watoto 6 Wachanga Wanafariki kila Saa 2 ndani ya Yemen!

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Licha ya majanga makubwa ya kibinadamu ndani ya Yemen kutokana na vita vilivyopelekea umasikini, ukame, kipindupindu, ukosefu wa huduma za afya na kusambaratika kwa kizazi chote, waamuzi katika usimamizi wa vita hivi wamefaulu japo kwa uchache kuweza kuwahadaa watu kuwa huu ni mzozo wa kindani katika eneo na kwamba unaendelea kuzidisha majanga ili kuweza kuwawekea pazia pande husika. Hii inaonyesha kiasi ya kutengwa na kutepetewa kwa suala la Yemen, ambalo limeingia mwaka wake wa nne katika “vita vya kimaslahi,” na imetoa kafara damu na maisha ya watu na mamilioni kufurushwa na wagonjwa kufikia kiwango cha kukata tamaa.

Yemen, Enyi Waislamu ni ardhi ambayo mama na watoto 6 wachanga wanafariki kila saa mbili kutokana na mimba na kujifungua kwa sababu ya ukosefu wa usimamizi wa afya, usafi, kuenea kwa maradhi, umasikini na ukame kwa kuwa ni nchi masikini katika Mashariki ya Kati!

Yemen, Enyi Waislamu inapakana na dola za Ghuba ambazo haziitambui kuwa ni sehemu ya GCC licha ya kwamba ina mzozo wa kimipaka na jirani Ufalme wa Saudi Arabia na Oman. Bali utiifu kwa Kafir Mmagharibi umeifanya Ufalme wa Saudi kwa maagizo ya Amerika kuongoza muungano wa kijeshi dhidi ya Yemen kwa kuivamia kijeshi pamoja na UAE, Oman na Qatar kabla ya kutolewa katika muungano huo! Watawala wa nchi hizo tulizozitaja na watawala wa Iran na watawala Yemen kaskazini na kusini wameshiriki katika kila aina ya uhalifu ambao umesibu watu wetu wa Yemen.

Yemen, Enyi Waislamu ni sehemu ya Ummah huu mmoja na tunaungana nayo kiAqeeda, kidamu, kicheo na kimatukufu na sio suala la kusahauliwa au kuzembewa hata kidogo, kiasi kwamba watu watazembea na kusahau janga lake na watu wake na kwa maisha ya watu wake, watoto, wanawake na wazee. Wakati huo huo majumba yanafunguliwa kwa ajiili ya mapaka na maumbwa duniani, mama na watoto sita wachanga wanakufa kila saa mbili ndani ya Yemen kutokana na njaa na maradhi. Je hili sio suala la kutia motisha wanaume na kuunganisha watu ili kutabban masuala ya Ummah na kuwaunganisha katika matatizo yao na kutafuta suluhisho lake?

Suluhisho la Yemen sio kwa kutafuta misaada ya kifedha kimataifa kama inavyopigiwa debe na UNICEF, mashirika ya misaada na Umoja wa Mataifa. Wamethibitisha dori yao ya kutiliwa shaka katika utekelezwaji wa ajenda za Kafir Mmagharibi. Ni aibu, kutamausha na kituko kuielekea Ulaya na Ikulu ya White House ili kuingilia kati na kupunguza janga hilo au kutangaza kuingilia kati kwa upole ili kusitisha janga hilo.

Ni fedheha kuona kwamba hayo ndiyo matakwa yetu ilhali Ummah wetu una majeshi ya kutosha na yenye uwezo wa kutatua suala la Yemen, Palestina, Syria, Iraq, Turkestan Mashariki, Myanmar na masuala mengine ya Ummah huu yakijumuishwa!!

Sisi sio Ummah usiokuwa na jeshi au utajiri kiasi kwamba tuweze kusimama mbele ya Magharibi na kuomba msaada na utajiri wao. Lau kuhodhi utajiri pasina mahitaji kumeharamishwa katika Uislamu na je kuhodhi silaha na majeshi ilhali tunayahitaji?! Majeshi haya yanabeba vyeo vikubwa duniani kinguvu za jeshi na wanaopigana kwa ujasiri na umahiri mkubwa lakini ni aibu kwamba yanashiriki katika uhalifu unaofanyiwa Yemen.

Janga la vifo vya kina mama na watoto wachanga kutokana na vita, umasikini, ukame, kipindupindu, ukosefu wa makaazi, kufurushwa na kila msiba ambao umeathiri watu wa Yemen unaweza kusuluhishwa kwa kutumia nguvu na ulinzi ambao utawalinda na kuwahifadhi wao kutokana na uovu kupitia jeshi kubwa ambalo litaokoa damu, hadhi, matukufu na kueneza amani, usalama na utulivu ndani ya dola kubwa na yenye nguvu! Hii ni Khilafah Rashidah ya pili kwa njia ya Utume, ambayo Hizb ut Tahrir inafanya kazi kwa ajili yake.

Yemen, Enyi Waislamu ni moja katika kadhia za Ummah huu na hatutakiwi kuipuza na kuisahau, kwa kisingizio cha misiba mingi inayotuzunguka kwani Waislamu ni Ummah mmoja tofauti na watu wengine na Mtume (saw) alisema: «إِذَا مَرَّ بِكُمْ أَهْلُ الْيَمَنِ يَسُوقُونَ نِسَاءَهُمْ، وَيَحْمِلُونَ أَبْنَاءَهُمْ عَلَى عَوَاتِقِهِمْ، فَإِنَّهُمْ مِنِّي، وَأَنَا مِنْهُمْ» “Lau mutawaona watu wa Yemen mnapishana nao huku wakiwa na wake zao na wamebeba watoto wao katika mabega yao, basi wao wanatokana na mimi na Mimi ni miongoni mwao”

**Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Nidhamu ya Elimu ya Msingi Katika Khilafah ya Uthman

Kampeni mbaya dhidi ya Waislamu na Uislamu zimekuwepo tangu kuteremshwa kwa Aya ya kwanza ya Quran. Yaliyokuwa madai ya kawaida zaidi ni yale yaliyotolewa na wale wanaotamani kuushambulia mtazamo wa Uislamu juu ya maisha ni kwamba mafunzo ya Uislamu yanapigia debe ujinga, ufuataji wa kipofu, kujenga watu wasiojali wenzi wao na wasio heshimu maendeleo ya kiteknolojia na kijamii hususan masuala yanayohusiana na wasichana na kuwawezesha kupitia elimu.

Lakini lau tutatathmini kwa makini ushahidi wa kihistoria kwa uadilifu tutaona kwamba Nidhamu ya Kisiasa ya Kiislamu imeipa elimu na kusoma kipaombelea cha juu kwa wanaume na wanawake.
Uislamu unapigia debe ufahamu safi kwamba kutafuta elimu ni kitendo cha ibada ambacho kitanyanyua daraja ya mtu hapa duniani na kesho akhera.

أَمَّنْ هُوَ قَانِتٌ آنَاءَ اللَّيْلِ سَاجِدًا وَقَائِمًا يَحْذَرُ الْآخِرَةَ وَيَرْجُو رَحْمَةَ رَبِّهِ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَالَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ

"Je! Afanyae ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama akitahadhari na Akhera, na akitarajia rehema za Mola wake Mlezi? Sema: Ati watakuwa sawa wale wanaojua na wasio jua? Hakika wanao kumbuka ni watu wenye akili." [Azzumar: 9]

Ni ruwaza hii ya mafanikio ndio iliyo wasukuma watawala wa Kiislamu ili kushajiisha masomo kwa wengi ili kuweza kuifahamu Quran na Sunnah. Dola ya Kiislamu ya kwanza ndani ya Madina iliasisi tamaduni ya kusomesha ummah tangu mwanzoni ulipojengwa Msikiti wa Mtume ambao ulitumika kama sehemu ya kuwafunza wadogo na wakubwa pamoja na kuwa ndio kituo msingi cha mujtama kwa jamii ya Waislamu.

Jukumu la Uislamu la kusomesha lilipelekea kuanzishwa kwa Chuo cha Kiislamu cha kwanza duniani kiitwacho Al Qarawiyyin katika mji wa Fez, Morocco.

Harakati za uvumbuzi katika elimu zilizifanya ardhi za Waislamu kuwa ndio kiongozi wa dunia katika nyanja za maarifa na usomi, kwa kiasi kikubwa mpaka watu muhimu kutoka nje ya ardhi za Waislamu walitaka kusomesha raia wao ndani ya Dola ya Khilafah katika zama tofauti tofauti za historia. Khilafah ya hivi majuzi ni ile ya Uthman ndani ya Uturuki, ilikuwa na mpagilio wa elimu ambao ulikuwa unashindana na wa taasisi nyingi zilizopo leo. Kwa mujibu wa Bwana Paul Ricaut (Muingereza Mwanadiplomasia, mwanahistoria na mjuzi kuhusu Ufalme wa Uthman), "Nidhamu ya elimu na kuadhibu ya Waturuki ni moja katika nguvu zao muhimu za siasa na ambazo zinamakinisha ufalme. Katika nidhamu hii si utajiri wala hongo wala si utabaka wa juu au ukaribu hauangaliwi, isipokuwa kinachotizamwa ni wema, umakinifu, uwajibikaji na tabia njema. Sultan mwenyewe amesimama kwa msingi wa sifa hizi."

Tukizingatia kuwa miaka 600 ya Khilafah ya Uthman ilijumuisha kilomita mraba milioni 14 za ardhi ambazo zilijumuisha Waturuki wa Cypriot, Wagiriki, Wabulgeria, Wapomak, Wasabia, Wakrosia, Wamontenegro, Wabosnia, Waablania, Wahangari, Wapole, Warumi, Waarmenia, Wajojia, Wasyria, Wachaldi, Waarabu, Waromania, Wafursi, Wakurdi, Wakopti, Waithiopia na Wabarbar, matamshi ya Ricaut yanadhihirisha kiukweli namna nidhamu ya elimu ya Khilafah ilikuwa ni yenye kujumuisha ambapo fursa ya mtu kusoma na kujiboresha haikukatazwa mtu, tatizo ambalo mpangilio wa kisiasa uliopo leo umeshindwa kulitatua kwa ukamilifu. Pamoja na mchanganyiko huo mkubwa wa jamii na tamaduni chini ya mamlaka moja pia tunao namna nidhamu ya elimu ya Kiislamu ilikuwa ni kiunganishi kikubwa kwa kuwa utaifa hauna thamani katika mfumo wa Kiislamu, aya kutoka katika Quran ilifundisha hivyo:

يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُم مِّن ذَكَرٍ وَأُنثَى وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ اللَّهِ أَتْقَاكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ

"Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa mataifa na makabila ili mjuane (SIO KWAMBA MCHUKIANE)." [Hujuraat: 13]

وَمِنْ آيَاتِهِ خَلْقُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافُ أَلْسِنَتِكُمْ وَأَلْوَانِكُمْ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّلْعَالِمِينَ

"Na katika Ishara zake ni kuumba mbingu na ardhi, na kutafautiana ndimi zenu na rangi zenu. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa wajuzi." [Ar-Rum: 22]

Huku akili changa zikitambulishwa fikra aina hizo, utambulisho ulijengwa kuanzia katika umri mdogo kuweza kuwa na uvumilivu na ubinadamu kwa watu wote kwa kuwa wameunganishwa kama raia wa Khilafah. Kwa hivyo ushindani na chuki za kidini zilikuwa kwa kiwango cha chini ambayo ilipelekea mujtama kuwa salama na usiokuwa na madhara.

Tathmini ya elimu ya Msingi pekee itadhihirisha namna kiukweli Uongozi wa Khilafah ya Uthman ulikuwa uko kipaombele katika kuhakikisha kunapatikana nafasi ya kivitendo ya elimu yenye kusifiwa kwa watoto wachanga ambao wako katika usimamizi wao. Katika Khilafah ya Uthman shule ilianza umri wa miaka 3 katika zile zijulikanazo kama Shule (Mektepleri) za Msingi (Sibyan)

Katika makala yake iliyochapishwa katika Jarida la Kimataifa la Watu na Sayansi ya Kijamii mnamo 2013, Professa Dkt Selami Sonmez wa Chuo cha Ataturk kutoka Uturuki aliorodhesha malengo ya elimu ya Msingi katika Khilafah ya Uthman kama ifuatavyo:

1. Kufundisha watoto wa Waturuki na Waislamu kusoma Quran kwa ufasaha na kuandika kwa Kiarabu vizuri
2. Kufundisha mambo ya msingi ya Uislamu
3. Kufundisha aina za ibada katika Uislamu
4. Kufundisha misingi ya maadili katika Uislamu na tamaduni.
5. Kuwasilisha na kufundisha maadili ya kweli ya Kiislamu.
6. Kutambua uwezo wa watoto
7. Kuandaa wanafunzi kwa Madrasa

Shule ima zilidhaminiwa moja kwa moja na serikali yenyewe au zilijengwa na kufadhiliwa na watu matajiri au makundi ya kijamii yakishirikiana kuelimisha vijana. Ilikuwa si jambo la ajabu kuona shule hizo zikifungamanishwa na msikiti wenyewe.

*Endelea Uk..7*

Ergin Osman katika kitabu chake cha 1977 cha, Historia ya Elimu ya Uturuki, aliandika kuwa ilikuwa ni umuhimu mkubwa kuelimisha kila nyanja ya jamii kwa serikali ya Uthman kiasi kwamba Fatih Sultan Mehmet alianzisha fikra ya kuweka kiwango maalum cha shule ambazo ziliruhudu watoto kutoka katika familia masikini au mayatima kuweza kuhudhuria ili kuhakikisha kuwa hakuna mtu yeyote asiyejiweza anakosa haki ya kupata elimu. Akaweka kanuni rasmi za elimu ya shule ya Msingi:

a. Elimu katika Shule za Msingi zilikuwa bure.
b. Matumizi ya kila siku ya 2 akche yalipeanwa.
c. Nguo, fez, shati, suruali, mikanda, viatu na kofia ziligawanywa kwa watoto wote.
d. Chakula kilipeanwa.
e. Safari iliandaliwa kila mwaka.

Ilikuwa sio jambo la ajabu kwa familia tajiri kudhamini watoto masikini hivyo basi kupelekea uwiano wa mujtama katika Dola ya Kiislamu.

Pia akataja kuwa siku ya kwanza kwa mtoto shuleni ilikuwa ni jambo kubwa la kijamii na kithaqafa kiasi kwamba wazazi, matajiri na masikini wangeli andaa sherehe maalum na maonyesho ya mtaani ili kusherehekea tukio hilo adhimu. Tamko rasmi la tukio hilo lilijulikana kama “ Maonyesho ya Amen ya Watoto.” Ahmed Rasim katika kazi yake ya 1927 ya Falaka. Istanbul imeelezea kwa undani sherehe hiyo kama iliyo jumuisha kuwalisha ndugu na marafiki na mtoto kutuzwa zawadi na kuvalishwa nguo mpya nzuri na dua kutolewa kwa mafanikio yao.

Mpangilio kabambe wa sherehe hiyo ya siku ya kwanza kwa mtoto shuleni ilikuwa na dori muhimu katika mujtama ifuatavyo:

a. Kushajiisha wazazi ili wawapeleke watoto wao shuleni
b. Kushajiisha mababa wa watoto walioko karibu na shule ili wawapeleke watoto wao shule
c. Kushajiisha mtoto kuanza shule
d. Kushajiisha kina dada na kaka walio na umri mkubwa pamoja na watoto majirani kuanza shule
e. Kupeana hadhi kwa familia ya mtoto

Osman Ergin ana nukuliwa katika utafiti wake wa 1977 uliofichua kwamba umuhimu wa shule kwa mujtama hauwezi kupatikana “ndani ya taifa lolote katika historia yake ya elimu!”

Dkt Selami Sonmez (2013) ameandika kwamba mbinu za mafunzo zilikuwa nyepesi ili kuweza kuruhusu watoto kusoma kwa kadri ya uwezo wao na watoto waliokuwa na uwezo zaidi waliruhusiwa kusonga mbele mara moja na wasiokuwa na uwezo walitengewa muda zaidi ili kuweza kufaulu. Madarasa makubwa yalisaidiwa na wanafunzi mahiri ambao walichaguliwa kama ‘wasomeshaji wasaidizi’ kwa wanafunzi wengine, hali ambayo imeigwa sasa na nidhamu ya shule za magharibi.


Kwa mujibu wa ushahidi wa kihistoria na kijamii ambao upo tunaweza kuhitimisha kwamba mpango wa elimu ya Msingi wa Khilafah ya Uthman unafichua wazi kwa ukamilifu uongo wa eti nidhamu ya kisiasa ya Kiislamu haina heshima kwa elimu, maendeleo na uelimishaji wa wasichana. Kinyume chake ni kwamba vikwazo vilivyoko katika kuweza kupata elimu kwa raia wanaoishi katika nchi zilizo kuwa kidemokrasia kutokana na utajiri, jinsia, kabila na utabaka vinajulikana na mataifa yote ya kimagharibi yanakumbana na janga hilo linaloendelea ambalo ni kuweza kuweka usawa wa kiukweli kwa raia wake. Katika mwaka huo huo wa 2013 katika makala iliyotajwa hapo awali, Dkt Selami Sonmez alinukuu kwamba sifa nzuri za Nidhamu ya Elimu ya Khilafah ya Uthman zilikuwa:

“... hata kwa dunia ya leo, sifa na dori ya Shule ya Msingi… ni jambo la ziada, na zipo nchi nyingi ambazo hazijafikia kiwango hicho.” (Nidhamu ya Elimu ya Msingi ndani ya Ufalme wa Uthman, Professa MsaidizI Dkt Selami Sonmez Chuo cha Ataturk 2013)

Tukijihami na elimu hii sasa tunaweza kutathmini khofu yetu ya kurudi tena kwa nidhamu ya Kiutawala wa Siasa ya Kiislamu na badala yake tubebe ruwaza njema, iliyojaa matumaini na kushajiisha watu wote kutokana na uwezo wake mkubwa wa kunyanyua wanadamu kwa kurudi tena Khilafah, Dola ya Kiislamu.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Imrana Mohammed**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**



# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 23: Ulazima wa Jihad na Udharura wa Kutumia Nguvu za Kimada ili Kuondoa Vizuizi Ambavyo Vinazuia Uislamu Usisambae

Hakika jambo linalokubalika kiakili, na linalojulikana wazi kabisa, bali linalojulikana katika dini ulazima wake, na kuwa kila itikadi (Aqidah) na kila mfumo wale walioubeba wanapotaka uendelee na uwe katika maisha hapana budi kupatikane nguvu itakayo unusuru na kuuhami na kuuhifadhi ili ubakie kuwa hai katika nyoyo za wafuasi wake, na uliovama wenye nguvu katika nyoyo za watu wake na wenye kuunga mkono, na kisha hunyenyekea watu wengine waliobakia. Na dalili juu ya hayo ni katika Qur'an na Sunnah:

Kwanza katika Qur'an: Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ تُرْهِبُونَ بِهِ عَدُوَّ اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ وَآخَرِينَ مِنْ دُونِهِمْ لَا تَعْلَمُونَهُمُ اللَّهُ يَعْلَمُهُمْ ۚ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ شَيْءٍ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يُوَفَّ إِلَيْكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُونَ

"Basi waandalieni nguvu kama muwezavyo, na kwa farasi walio fungwa tayari-tayari, ili kuwatishia maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu, na wengineo ambao hamuwajui, lakini Mwenyezi Mungu anawajua. Na mkitoa chochote katika Njia ya Mwenyezi Mungu mtarudishiwa, na wala nyinyi hamtadhulumiwa." [An-Anfal: 60]

Na ushahidi bora kabisa ya kwamba nguvu ni lazima ili kuusambaza mfumo, ni ufunguzi (fat'hu) wa Makkah. Siku Mtume (saw) alipoifungua Makkah, ilikuwa kabla ya hapo watu wanaingia katika Dini wawili watatu.

Ama watu walipoona nguvu na nusra ya Mwenyezi Mungu na ufunguzi ikawa watu wanaingia katika Dini yake makundi kwa makundi. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ، وَرَأَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُونَ فِي دِينِ اللَّهِ أَفْوَاجًا فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَاسْتَغْفِرْهُ ۚ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا

Itakapo kuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi, Na ukaona watu wanaingia katika Dini ya Mwenyezi Mungu kwa makundi, Zitakase sifa za Mola wako Mlezi, na umwombe msamaha; hakika Yeye ndiye anaye pokea toba. [An-Nasr: 1-3]

Mwenyezi Mungu (swt) asema:

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ ۖ وَأَنْزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنَافِعُ لِلنَّاسِ وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ وَرُسُلَهُ بِالْغَيْبِ ۚ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ

"Kwa hakika tuliwatuma Mitume wetu kwa dalili waziwazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na Mizani, ili watu wasimamie uadilifu, na tumeteremsha chuma chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu, na ili Mwenyezi Mungu amjue anaye mnusuru Yeye na Mitume wake kwa ghaibu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye kushinda." [Al-Hadid: 25]

Mazingatio ni kuwa Mwenyezi Mungu (swt) anatupa habari kuwa Yeye alituma mitume kwa hoja zilizo wazi, na akawapa vitabu, akaweka mizani katika ardhi ili watu wanyooke na wafuate njia Yake ambayo itawahakikishia uadilifu na usawa katika maisha ya dunia. Lakini (swt) aliyetukuka Mwenye hikma ya juu anajua kuwa watu hawawezi kukubali da'wah ya haki kwa wepesi na usahali huu, basi hapana budi kupatikane nguvu ambayo itakuwa pamoja na hiyo mitume na hivyo vitabu.

Hapana budi Da'wah ya haki iwe na nguvu itakayoihami na kuinusuru; ndio Mwenyezi Mungu (swt) akafunganisha uteremshaji wa Qur'an na mizani pamoja na chuma, na akataja kuwa ndani ya chuma kuna nguvu nyingi, kisha mwisho wa Aya akataja kuwa Yeye (swt) ni Mwenye nguvu mshindi.

Khalifa wa tatu Uthman ibn Affan (ra) ametafsiri hii maana aliposema: [Hakika Mwenyezi Mungu anaondoa kwa Utawala (sultan) ambayo hayaondolewi kwa Qur'an (mawaidha pekee)]

Pili katika Sunnah: amepokea Bukhari katika Sahih yake

*Endelea Uk..9*



Email: info@uqab.or.ke

kuwa Mtume (saw) alisema: (Nimeamrishwa nipigane na watu mpaka waseme: LAA ILAAH ILLA LLAH MUHAMMAD RASULULLAH, Watakapoyasema maneno haya, nami nitalinda mali yao na damu yao isipokuwa kwa haki yake)

Miongoni mwa vitendo vya Mtume (saw) ni kitendo cha kwenda mbio kutafuta nusra kwa watu wenye nguvu na mamlaka. Kwani alikuwa (saw) akitafuta nguvu ambayo itaisukuma da'wah ya haki na itakayomhami ili aweze kufikisha aliyoamrishwa na Mwenyezi Mungu (swt).

Na kisha inashuhudiwa katika historia kuwa popote ambapo watu wananyimwa haki zao, na miji yao kutekwa haitaweza kurudi kwa watu wake ila kwa nguvu.

Asema mshairi kuwaambia Ummah:

يا أمة لخصوم ضدها احتكمت

Ee Ummah unaotaka kuhukumiwa na hasimu wake

كيف ارتضيت خصيما ظالما حكيما

Vipi umeridhia hasimu dhalimu awe hakimu?

بالمدفع استشهدي ان كنت ناطقة

Pata shahada kwa kupigwa kombora ukiwa mkweli

أو رمت أن تسمعي من يشتكي الصمما

Ama ushawahi kusikia mtu anapeleka mashtaka kwa kiziwi?

افـرع له خيراتلاو ثداوحلا يلس

Yaulize matukio na historia je, mnajua

حقا ورأيا بغير القوة احترما؟

Haki yoyote ama rai iliyowahi kuheshimiwa bila ya kuwepo na nguvu?

لا تطلبي من يد الجبار مرحمة

Usitafute huruma kutoka kwa mikono ya bepari

ضعي على هامة جبارة قدما

Weka unyayo juu ya kichwa cha bepari

Miji ya Waislamu ikiwemo Palestina n.k iliyotekwa na mabepari na hivi sasa inahukumuiwa kwa mujibu wa mfumo wa kikafiri wa kisekula wa kirasilimali. Kwa hivyo inahitaji nguvu ili iweze kukombolewa kutoka katika kiza na kuingia katika nuru ya Uislamu.

# SWALI/JAWABU: Uhalisia wa Uhasama Kati ya Marekani na Iran Katika Eneo Hilo



**Swali:**

Amerika ghafla imetangaza hatari kwa vikosi vyake na maslahi yake katika eneo la Ghuba, inayotoka kwa Iran na vikundi vyenye mafungamano nayo; ilikuza kiwango cha utayari na kutuma meli ya kijeshi na yenye kubeba ndege, na hata kutuma hospitali ya wanamaji ikiashiria kukaribia kwa makabiliano katika Ghuba. Hii ili sadifiana na kumalizika kwa sera ya Amerika ya kuzitenga nchi zinazo agiza mafuta ya Iran ili kukomesha usafirishaji mafuta ya Iran. Iran imetishia kufunga Mwanya (strait) wa Hormuz kwa nchi zote za Ghuba zinazo safirisha mafuta kupitia hapo huku uhasama ukiendelea eneo hilo! Je huu ndio mwanzo wa vita vitakavyo anzishwa na Amerika katika eneo hili? Ama kuna lengo jengine? Mwenyezi Mungu akujaze kheri.

**Jawabu:**

Ili kufafanua taswira kamili, turegelea kadhia zifuatazo:

1- Hakika, kuna ongezeko kubwa la uhasama katika eneo hilo, ikiwemo kile kilicho tajwa kupelekwa kwa vyombo vya kivita vya majini vya Marekani, ikiwemo Lincoln aircraft carrier, meli kubwa zaidi inayobeba ndege 90 za kivita na ikatuma kikundi cha B-52 kwenye ngome zake katika maeneo ya Ghuba hilo, ikiongeza tahadhari miongoni mwa vikosi vyake na kuondoa wafanyi kazi wasio na umuhimu sana katika ubalozi wao ulio Baghdad. Kile kilicho shuhudiwa ni kufuatishwa tishio la haraka kwa Iran: [Marekani imetuma shehena za kivita mashariki ya kati kwa Iran "ujumbe ulio wa wazi na bila kukoseka.'' Mshauri wa masuala ya kiusalama John Bolton amesema nchi yake ilifanya hivyo "kujibu shida na ongezeko la mfano wake na onyo.'' "kutumwa kwa meli za kivita katika Ghuba kufuatia habari za uezekano wa uvamizi kwa vikosi vya Marekani, kulingana na wanahabari wa Reuters wakimnukuu afisa wa Marekani ambaye hakutajwa jina …... Bolton amesema katika kauli kuwa, "Marekani inatuma vikosi vya kushambulia viitwavyo USS Abraham Lincoln strike group na jopo kazi la ulipuaji mabomu kwa eneo la taasisi kuu ya utoaji amri za kijeshi kutuma ujumbe ulio wazi na usio na makosa kwa serikali ya Iran kuwa shambulizi lolote kwa maslahi ya Marekani na washirika wake litakabiliwa na nguvu zisizo na huruma.'' (BBC, 6/5/2019). Kiuhakika shehena za kubeba ndege ziliingia mkondo wa bahari wa Suez Canal tarehe 9/5/2019 na kisha kufika bahari Arabu mnamo 14/5/2019. Vyombo vya habari vimetangaza kuwa Marekani (yataka kutuma vikosi elfu 120 zaidi katika eneo hilo , habari ambazo zimekataliwa na Rais Trump wa Marekani, ingawa Kaimu Waziri wa Ulinzi Patrick Shanahan amefikisha pendekezo la mipango hiyo kwa Trump…( RT, 14/5/2019, ikinukuu gazeti la 'New York Times'), yote yaongezeka kwa muongezeko wa matishio kutoka Iran (CNN, ilinukuu chanzo chake, mnamo Mei 7, kwamba utawala wa Marekani umepata habari za kiupelelezi zioneshazo Iran inapanga kuweka zana za kurusha makombora ya masafa mafupi katika vyombo vyake vidogo katika Ghuba. (RT, 14/5/2019)

2- Kile kilichofanya mvutano wa Marekani kuwa zaidi ya maneno tu ni kilichofanyika kwa vyombo vinne vya kibiashara karibu na bandari ya Fujairah katika Imarati na shambulizi katika vituo muhimu vya mafuta katika nchi ya Ufalme wa Saudi na haya ndio yaliyofuatia:

A- [Vyombo vya kibiashara vinne karibu na maji ya Imarati vilihujumiwa bila ya majeraha yeyote, kulinga na kile Waziri wa Kigeni wa Imarati alisema Jumapili. Haya yametendeka kama shinikizo la Marekani juu ya Iran, ambayo Rais Hassan Rouhani amekubali mapema kuwa nchi yake inakumbwa na

*Endelea Uk..11*

hali ngumu. (Middle East Online 12/5/2019)]

B- [Kikundi cha Yemen "Ansar Allah" kimetangaza, Jumanne kuwa, kimefanya mashambulizi kutumia ndege zisizo na rubani katika vifaa muhimu vya Saudi… Chombo cha habari Al Masira kikinukuu chanzo cha kijeshi, kilithibitisha kwamba "ndege 7 zisizo na rubani zimevamia vifaa muhimu vya Saudi," chanzo kimeashiria kuwa "Uvamizi huu mkubwa umekuja kujibu ongezeko la fujo na hujuma kwa watu wetu," kuongezea kuwa "Ansar Allah wako tayari kutekeleza shambulizi maalum na baya zaidi kama fujo na hujuma zisizo za haki zitaendelea." (Sputnik Russian Agency, 14/5/2019)]. Kwa haya matokeo mawii, Kauli za Marekani zinakuja na hatari katika Ghuba hii na zimepata mazingira mazuri na mvutano wa Marekani na kukolea kwa hali hii ya Ghuba ni tofauti na matukio kama haya yaliyopita.

3- Hata hivyo, na mvutano huu wote eneo la Ghuba, linaashiria vita viko mlangoni, kauli za pande zote mbili, Amerika na Iran, zinapeana taswira nyingine, kwamba vita havitarajiwi! Kauli hizi ikiwemo;

- [Trump amesema katika kauli kwa vyombo vya habari siku ya Alhamisi, katika Ikulu yake, akijibu swali ikiwa Marekani imedhamiria kupigana na Iran: "natarajia haitatokea.'" (RT, 16/5/2019)]

- [(Reuters 16/5/2019) Spika wa Bunge la Seneti wa Marekani Nancy Pelosi alisema siku ya Alhamis kwamba utawala wa Trump hauna idhini kutoka kwa bunge la Congress kuanzisha vita dhidi ya Iran, huku kukishuhudiwa muongezeko wa mvutano katika Mashariki ya Kati. Pelosi amewaambia wanahabari kuwa utawala wa Republican utatoa kauli baada ya mkutano wa ndani wa wakuu wa chama hicho wajulikanao kama 'Gang of eight', juu ya Iran siku ya Alhamisi.]

- [(Reuters 16/5/2019) New York Times ilisema mnamo Alhamis, wakinukuu maafisa ambao hawakutajwa jina, katika utawala wa Marekani - Raisi Trump amemwambia Kaimu Waziri wa Usalama Patrick Shanahan kwamba hataki mapambano ya kivita na Iran. Hilo gazeti lilisema kwamba Rais amemwambia Shanahan hivyo Jumatano asubuhi).

- [(Kiongozi mkuu wa Iran Ali Khamenei amesema hakutakuwa na vita na Marekani, katika maoni yaliyo chapishwa katika chombo cha habari cha serikali na katika mtandao wake wa kijamii wa Twitter, Ayatollah Ali Khamenei alisema, "hatutafuti vita, wala hawavitafuti." (BBC, 14/5/2019)]

- [(Mshikilizi wa wizara ya usalama wa Marekani, Patrick, aliliambia kongamano la wanahabari kuwa, lengo la utawala wa Marekani la kuthibitisha uwepo wake wa kivita katika Ghuba ya Arabu ni kuzuia wala si vita." (France 24, 22/5/2019)] mwisho wa nukuu

Kauli hizi za Marekani na Iran zinaashiria kile kinacho tangazwa na vyombo vya habari, kuhusu vita kati ya Amerika na Iran si hakika. Kile alichokisema kiongozi wa Iran kwa watu wake ni, wala hawatafuti vita wala wao hawavitafuti, ndio kauli yenye uzito. Hii ni kulingana na kauli kuhusiana na vita, na kuharibiwa kwa meli za kivita za Marekani limetengwa. Na katika matarajio yaliyo kithiri, kama vita vitatokea, vitafungika katika kutetea muonekano wa pande hizo mbili. Kauli za viongozi wa Marekani mara kwa mara ni kwamba hawataki kubadilisha utawala. Mshauri wa masuala ya Usalama wa marekani, John Bolton, amesema: (sera zetu hazilengi kubadilisha utawala wa Iran, lakini tunataka kuweka shinikizo lisilo la kawaida kwa serikali ya Iran ibadili mwenendo''... (Tovuti ya Ad-Dustoor 3/10/2018)

4- Kwa hivyo ni ipi sababu ya kuongezeka mvutano eneo hili? Jawabu liko katika sababu tatu zifuatazo:

**Sababu ya kwanza ni soko la mafuta la kiulimwangu:** Mtazamo wa Marekani kuhusu suala la mafuta umebadilika tofauti na Karne iliyopita, tangu kufanikiwa kwa utafiti wa kuchimba mafuta ya Shale, na Kuruhusu uuzaji wake katika masoko ya nje hata kama inaagiza mafuta kutoka nje na ili kuweka sawa mizani ya biashara na Uchina ni wazidishe uagizaji wa mafuta ya Marekani. Wakati huo huo Marekani inaagizia mafuta kwa bei rahisi kwa viongozi dhalili wa mataifa ya Ghuba, hasa utawala wa Saudi, ambao pesa zake zimerundikana Marekani bila ya kuwa na uwezo wa kuziondoa mpaka mahitaji yatokee, kwa hivyo wanakopa ilhali pesa zao wenyewe hawawezi kuzitumia. Kulingana na hali halisi, shinikizo la Marekani juu ya Iran na kukatazwa kuuza mafuta katika soko la nje itapandisha gharama za mafuta kiulimwengu na hili litafaidi Marekani, kama kuongezeka bei ya mafuta ni mazingira mazuri kwa gharama ya uzalishaji wa mafuta ya Shale. Shirika la Kimataifa la Nishati lazungumzia kuhusu kuchochewa na "kuchanganyikiwa na muonekano wa ugavi" wa mafuta na imeongea kuhusu uwezo wa Amerika kufidia kupungua kwa ugavi wa mafuta kutoka Iran na Venezuela. [(Shirika la Ulimwengu la Nishati lilisema mnamo Jumatano kwamba dunia inahitaji ugavi mdogo wa ziada wa mafuta kutoka OPEC mwaka huu, kwa kuwa Marekani itafidia pengo la uzalishaji litakalotokana na Iran na Venezuela kutosafirisha mafuta yao nje. (Reuters,15/5/2019)] sawia na [(Shirika la Ulimwengu la Nishati limesema, uchimbaji mafuta Marekani kutoka mawe makuu saba utazidi mpaka kufikia mapipa milioni 8.49 kwa siku kufikia mwezi wa Juni. (Reuters,17/5/2019) hivyo ni kuwa kampuni za mafuta za Marekani zinachimba mafuta zaidi wakati wa kuzidi mvutano wa Ghuba huku inazorotesha uchimbaji wa mafuta ya Iran kupitia vikwazo.

Muhimu zaidi, bei ya mafuta inapanda huku Amerika ikitishia kuhujumu vifaa na meli za kubeba mafuta (Tathmini ya Mafuta ilipanda baadaye, Jumatano huku kukiwa na kuzidi kwa mvutano Mashariki ya Kati, unaathiri ugavi wa mafuta ulimwenguni, ikikuza ongezeko la wawekezaji wa biashara ya mafuta iliyokuwa haikutarajiwa. Bei ya mafuta imepanda na senti 53 ama asilimia 0.7, kufikia dola 71.77 kwa kila pipa, ilhali bei ya mafuta ya Marekani kuuzwa dola 62.02 kwa kila pipa, kupanda kwa senti 24 ama asilimia 0.4. Bei za mafuta imepigwa jeki baada ya Saudi kusema Jumanne kwamba ndege zisizo na rubani zimelipua mabomba mawili ya mafuta siku mbili baada ya hujuma kwa meli za mafuta karibu na Imarati. (Reuters 05/15/2019).

Hivyo, iko wazi kuwa Amerika inafaidi katika mvutano huu kati yake na Iran kwa kuongezeka bei ya mafuta na imeweza kuongeza uchimbaji wa mafuta, kampuni za Amerika zimekimbilia kuchimba mafuta zaidi ya Shale kwa viwango ambavyo havikutarajiwa. Hakuna shaka kuwa Amerika inatizama mvutano huu kama faida kwa kampuni zake za mafuta haswa ni mtazamo wa fikra za kibiashara zinazo tawala mabongo ya uongozi wa Trump.

**Sababu ya pili: Kuingia kwa makubaliano mapya ya kinyuklia na Iran, kutadhamini mgao mkubwa wa faida kwa**

*Endelea Uk..12*

**kampuni za Amerika katika soko la Iran.**

Inajulikana vizuri kwamba Amerika inacheza mchezo wa wazi na Iran ili kuingia kwa makubaliano mapya ya kinyuklia, ikiwemo mpango wake wa makombora na ushawishi wake katika eneo. Wakati Waziri wa Kigeni wa serikali ya Amerika alipozuru nchi ya Iraq, Kile Pompeo alicho mwambia Abdul Mahdi kiukweli, kulingana na vyanzo vinavyo jua kwa undani kuhusu mkutano wao, ilikuwa tofauti kabisa na hata Waziri Mkuu wa Iraq alishangazwa na vile Pompeo alivyo ongea naye. Pompeo alimwambia kuwa afikishe salamu Tehran kwamba Amerika haiko makini na vita na kile Trump anataka ni makubaliano mapya ya kinyuklia – makubaliano ambayo yana sifa zake mwenyewe… Noon Post 15/05/2019, nukuu British Middle East Eye). Na Rais wa Amerika hafichi lengo lake: (Rais wa Amerika aelezea hisia zake za kuwasiliana na Iran kumaliza mvutano, ambao unazidi kuwa tete, na uongozi ukaacha nambari za simu kwa Uswizi ili Iran iweze kuwasiliana nao ili wakubaliane. Rais wa Amerika amesema, "kile wanahitajika kufanya ni waniiite, tukae chini na tuweze kukubaliana, makubaliano bora." Trump amesema, "Hatutaki tu, wawe na silaha za kinyuklia. Hatutaki mambo mengi, na tutawasaidia kuwaweka katika hali bora zaidi, hatutaki kuumiza Iran," Trump amesema katika hotuba aliyoitoa Ikulu. "Nataka wawe na nguvu kubwa na wawe na uchumi mkubwa lakini lazima watuite na wakituita tuko tayari kuongea nawo."

White House iliwacha nambari ya mawasiliano ya simu kwa Uswizi, ambayo inawakilisha Iran katika mahusiano ya kidiplomasia na Amerika, ili iwe daraja la mawasiliano ikiwa Tehran wanataka makubaliano na Washington (CNN, 11/05/2019). Vile vile kama RT walivyo ripoti 15/05/2019 kwamba Raisi wa Amerika Trump amesema yuko na uhakika kwamba Iran watataka makubaliano karibuni). Kwa mukhtadha huo huo, "Intikhab" Tovuti ya Iran iliyo karibu na wanamageuzi, umeweka wazi Jumanne malengo ya ziara ya Waziri wa Kigeni wa Oman Yusuf bin Alawe kwenda mji mkuu Tehran. Tovuti imesema 21/5/2019 kwamba (lengo la ziara ni kupatanisha kati ya Amerika na Iran na kujadili mada ya kulengwa ubalozi wa Amerika ulioko Baghdad na maendeleo ya eneo…) Tovuti ukaongezea kuwa (waziri wa Oman, Yusuf bin Alawe, amekuja pamoja nayo katika ziara hii ya ghafla salamu kutoka kwa Rais wa Amerika Donald Trump) bila kupeana maelezo ya ndani.

**Tatu, na la muhimu zaidi, ni mchakato wa kuunda muungano wa Amerika na Waarabu ambao utajumuisha umbile la Kiyahudu dhidi ya Iran.**

Ukiangalia malengo ya sera za Amerika katika eneo na msimamo wa eneo lenyewe, inaonyesha kwamba sababu muhimu ya Amerika kuongeza mvutano wake na Iran ni kujenga muungano na kuufanya rasmi. Hivyo ni kuhamisha mzozo wa eneo kutoka kwa uvamizi wa Israeli na kukaa kwake katika Ardhi tukufu ya Palestina ambayo lazima ipiganiwe na ikombolewe na irudishwe Palestina katika ardhi za Waislamu, mpaka kwa mzozo wa kimadhehebu dhidi ya Iran! Kwa maneno mengine, kujumuisha umbile la Kiyahudi katika eneo. Lengo hili, ambalo Amerika na Uingereza hazikufaulu kwa makarne, leo lina matumaini ya kufaulu kupitia viongozi wasaliti hasa wa eneo la Ghuba, ambao wanakimbilia kusawazisha na umbile la Kiyahudi chini ya kisingizio cha Amerika "hofu dhidi ya Iran".

Hili liko wazi katika msimamo wa Umbile la Kiyahudi: "Katika kivuli cha mvutano katika Ghuba, Waziri Mkuu wa umbile la Kiyahudi, katika uwepo wa balozi wa Amerika Friedman, amesema, "Kuna mwangaza mpya, mwamko mpya katika uhusiano wetu na nchi nyingi jirani zetu za Waarabu na nyingi za wasiokuwa Waarabu. Tumeunganishwa na hamu yetu ya kusimamisha uchokozi wa Iran. Israel na nchi zote katika eneo na nchi zote zenye kutafuta amani lazima zisimame pamoja na Amerika dhidi ya fujo za Iran. Lazima tuendelee kuimarisha taifa la Israel na kuendelea kuimarisha muungano wa lazima na Amerika.'' (RT 14/05/2019). Kwa umbile la Kiyahudi kusimama na Waarabu au pengine nchi za Kiislamu na Amerika kusimamisha uchokozi wa Iran, inaashiria kuwa mazungumzo ya mpango wa mvutano wa Amerika ni kuunda muungano wa eneo dhidi ya Iran, ikiongozwa na Amerika, ikiwemo kujumuishwa umbile la Kiyahudi kupitia mvutano huu, kauli za uchochezi na baadhi ya matendo ya kijeshi kama ilivyo Fujairah na vyombo vya Aramco ni mchakato wa kuzindua muungano huu wa NATO ya eneo na mchakato wa kuzindua hilo bado waendelea. Utangulizi wake ni kupokewa Riadh siku ya Jumatatu, 6/04/2019 kwa mkutano wa Waarabu na Amerika ambao Qatar ilihudhuria katika kuzindua Muungano wa Mikakati ya Mashariki ya Kati inayojulikana kama "NATO ya Kiarabu" katika vyombo vya habari. Shirika la Habari la Saudi limetangaza [mkutano umefanyika "kwa ushirika mkubwa wa Saudi, Amerika, Imarati, Ufalme wa Bahrain, nchi ya Kuwait, Usultani wa Omani, nchi ya Qatar na Ufalme wa Jordan." Mkutano umeeleza: "Ni hatua muhimu katika mchakato wa kuzindua huu muungano, ambao umedhamiria kuongeza usalama na utulivu katika eneo na duniani." (RT 10/04/209)]. Kwa hivyo, mchakato wa kujenga muungano huu wa kivita uko na nguvu zote. Furaha ya Umbile la Kiyahudi ya kuratibu usalama na Waarabu na nchi za "Kiislamu" dhidi ya Iran inamaanisha umbile la Kiyahudi litahusika katika maamuzi ya Amerika na sheria lakini bila ya tamko. Kutangazwa kwake kutachelewa mpaka Amerika ipange kwa amani na la muhimu kusawazisha viongozi wasaliti wa Ghuba na Umbile la Kiyahudi.

**Hitimisho**

1- Kuendelea kwa matukio na hali ya Mvutano sio mwanzo wa vita vya kina baina ya Amerika na Iran, lakini kuna uwezekano wa kufanikisha sababu tatu zilizo tajwa, lakini hili halitozuia mashambulizi madogo madogo kutokea ili kustiri muonekano wa pande hizi. Kuzuia kutoaibika kwa sababu ya mwenendo wao wa uchochezi na kauli zao za vitisho, kuzuia makosa yasitendeke na kubadilisha tabia!

2- Inaumiza kwamba hata kama Amerika haikuficha malengo yake katika semi na vitisho vyake, viongozi wa nchi zetu, haswa za eneo la Ghuba, wanahalalisha kiburi cha Amerika na utawala wake kwenye eneo, kana kwamba wao ni viziwi, mabubu na vipofu na hawaelewi na kisha wanaukosa huu ulimwengu na wa mwisho. Mwenyezi Mungu (swt) asema kweli:

وَمَنْ كَانَ فِي هَذِهِ أَعْمَى فَهُوَ فِي الْآخِرَةِ أَعْمَى وَأَضَلُّ سَبِيلاً

"Na aliye kuwa hapa kipofu, basi atakuwa kipofu Akhera, na atakuwa aliye ipotea zaidi njia" [Al-Isra': 72].

**19 Ramadan 1440 H**
**24/5/2019 M**



Email: info@uqab.or.ke